TANGAZO LA SERIKALI NA 529 la tarehe 21/9/2018

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA 290

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MASOKO ) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA, 2018

Jina na Mwanzo wa kuanza kutumika.

1 Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Masoko) za Halmashauri ya Wilaya ya Newala za mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2 Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Newala.

Tafsiri

3 Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:

*"Halmashauri"* maana yake Halmashauri ya Wilaya ya Newala,

*"Kamati ya soko"* maana yake ni kamati iliyoundwa na

wafanyabiashara katika soko ambayo kazi zake zimeanishwa

kwenye Sheria Ndogo hizi

*"Kibali"* maana yake ni idhini ya maandishi

inayotolewa na Mkuu wa

Masoko kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi;

*"Kizimba"* maana yake ni pamoja na umbo, meza, eneo,

kiwanja au sehemu yeyote katika soko inayotumika au

Iliyokusudiwa kutumika kwa ajili ya kuuza bidhaa.

*"Mfanyabiashara"* maana yake ni mtu yeyote anayeuza bidhaa

sokoni,gulioni kwa jumla au rejareja kwenye eneo ambalo

limeruhusiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"Mkuu wa soko" maana yake Afisa wa Halmashauri

aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia shughuli zote katika soko;

*"Mkurugenzi"* maana yake Mkurugenzi wa Halmashauri ya

Wilaya ya Newala au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza

majukumu ya Mkurugenzi

*Soko"* maana yake soko, gulio na minada inayomilikiwa na

Halmashauri;

*"Ushuru"* maana yake ni ushuru wa soko wa Halmashauri ya

Wilaya ya Newala unaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa Halmashauri

4 Halmashauri ina wajibu wa:-

a) kuanzisha, kusimamia na kuendesha masoko kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.
b) kuendeleza masoko yaliyopo.
c) kusimamia usafi na usalama wa masoko;na
d) kusimamia ufikishaji wa huduma za kijamii katika soko
e) kusajili wafanyabiashara wote katika masoko yote ya Halmashauri kwa kutumia fomu maalum kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.
f) ugawa na kupangisha katika soko vyumba, meza au vizimba ambavyo vitalipiwa ushuru kwa viwango vilivyooneshwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Mkuu wa Soko

5 Halmashauri itamteua Mkuu wa Masoko kwa ajili ya kusimamia shughuli za uendeshaji wa soko pamoja na:-

(a) kukusanya ada mbalimbali kama zilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza na la pili la Sheria Ndogo hizi.
(b) kuimarisha huduma za ulinzi, maji na umeme katika soko;
(c) kushirikiana na kamati ya soko, kuwasajili wadau wa soko.
(d) kusimamia usafi na uondoshaji wa taka katika soko;
(e) kuhakikisha biashara hazifanywi kwenye eneo ambalohaliruhusiwi kwa shughuli hiyo;na
(f) kutekeleza majukumu mengine yoyote atakayo agizwa na Halmashauri.

(g) kwa kushirikiana na Afisa Biashara na mapato Kusimamia magulio na minadayoteinayoendeshwa katika eneo la halmashauri.

Wafanyabiashara

6 Wafanyabiashara watasajiliwa na Mkuu wa Soko akishirikiana na Kamati ya Soko kwa lengo la kuwatambua na kuwaorodhesha kwenye rejesta maalum.

Wajibu wa Mfanyabiashara

7 Ni wajibu wa kila mfanyabiashara katika soko au gulio:-

a) kusajiliwa na Mkuu wa Soko katika rejista maalum ya soko.
b) kulinda na kuhifadhi miundombinu ya soko
c) kufanya biashara kwenye maeneo yanayo ruhusiwa.
d) kusimamia usafi katika eneo lake la biashara
e) kutojihusisha na shughuli za siasa katika eneo la soko
f) kuhakikisha analipa ushuru, kodi au ada anayodaiwa kwa wakati.
g) kubandika au kubandua tangazo kwa idhini ya mkuu wa soko
h) kutotumia lugha ya matusi, kuudhi au kashfa katika eneo la soko
i) kuheshimu masharti ya upangaji aliyopewa na Halmashauri.
j) kushiriki usafi wa soko

Kamati ya soko

8 (1) Kamati ya wadau wa soko itaundwa na wadau kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Wadau wa soko watakuwa ni mwakilishi mmoja kutoka kila kikundi cha Ushirika ndani ya soko

Kazi za kamati ya wadau wa soko

9 Kazi za Kamati ya wadau wa soko ni:-

(a) kuhakiki biashara na utendaji wa soko.
(b) kuboresha ustawi wa wanachama na vyama vya ushirika katika soko.
(c) kuhakikisha nidhamu katika shughuli za soko
(d) kuinua ustawi wa biashara katika soko.
(e)

Kamati ndogo

10 Kamati ya Wadau wa soko itaunda kamati ndogo

zenye wajumbe wa kamati wanne kutoka miongoni mwa wajumbe wa kamati ya wadau wa soko ambazo ni:-

(a) Kamati ndogo ya miundombinu na usafi
(b) Kamati ndogo ya utawala na biashara
(c) Kamati ndogo ya ulinzi na usalama

Vikao vya kamati ya soko

11 (1) Vikao vya kamati ya wadau wa soko vitafanyika mara moja kila mwezi.

(2) Mkuu wa Masoko atakuwa Katibu katika vikao vyote vya Kamati ya wadau wa soko.

Kibali

12 Wafanyabiashara wote watapewa kibali cha kufanya biashara katika soko husika kutoka kwa Mkuu wa Soko kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Utolewaji wa kibali kwa biashara ambazo hazikuwepo

13 (1) Mkuu wa Soko kwa kushirikiana na kamati ya wadau wa soko kwa idhini ya Halmashauri wanaweza kutoa kibali cha kufanya biashara ambayo awali haikuwepo au haikuwa na eneo ndani ya soko.

(2) Kibali hicho kitatolewa kwa muhusika baada ya kulipa ada na kitadumu kwa muda wa mwaka mmoja tangu siku ya kutolewa, na endapo mfanyabiashara atataka kuendelea na biashara katika soko, atatakiwa kuomba kibali kingine kwa Mkuu wa soko.

Kufuta kibali

14 Mkuu wa Soko anaweza kufuta kibali kilichotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi endapo mwenye kibali hicho:-

(a) atakuwa na malimbikizo ya kodi au ushuru
(b) atakuwa amesimamisha shughuli zake kwa mwezi mitatu bila taarifa.
(c) atakuwa amekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi hata baada ya kuonywa
(d) atawashawishi wafanyabiashara wengine kutofuata Sheria Ndogo hizi na kusababisha uvunjaji wa amani.

Saa za kazi

15 (1) Soko litakuwa wazi siku zote kuanzia saa kumi na

mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Mkuu wa Soko kwa kushirikiana na wadau wanaweza kufunga soko kwa ajili ya matengenezo na sababu nyingine yoyote ya dharura pale itakapo onekana inafaa ilimradi watoe taarifa ya maandishi kwa Mkurugenzi

(3) Kamati kwa kushirikiana na Mkuu wa Soko wanayo mamlaka ya kufunga soko kabla ya saa kumi na mbili jioni kutokana na mwenendo wa shughuli sokoni au kwa sababu zitazoainishwa.

Uteuzi wa wakala

16 (1) Halmashauri inaweza kumteua wakala ambaye atawajibika katika uendeshaji wa soko kwa niaba ya Halmashauri.

(2) Wakala atakayeteuliwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atasimamia shughuli za uendeshaji wa soko kwa kwa mujibu wa mkataba atakaoingia na Halmashauri.

Ushuru na kodi ya soko

17 (1) Halmashauri itatoza kodi au ushuru wa soko kutoka kwa kila mfanyabiashara aliyesajiliwa kufanya biashara katika eneo la soko kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

(2) Mfanyabiashara yeyote sokoni atatakiwa kulipa kodi,ada na ushuru kwa Halmashauri au wakala wake kama ilivyo oneshwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

Ushuru wa jokofu

18 Mtu yeyote atakayetumia chumba cha baridi au jokofu la soko kuhifadhia bidhaa atalipa ushuru kwa Halmashauri au wakala kwa ajili ya kutumia sehemu hiyo kama itakavyo amuliwa na Halmashauri.

Ushuru wa kupakua na kupakia mizigo

(1) Kutakuwa na ushuru utakao tozwa kwa kila gari litakaloingia ndani ya eneola soko au barabara za

soko kwa ajili ya kupakua au kupakia bidhaa kama ilivyo ainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

(2) Magari yataruhusiwa kuingia katika eneo la soko kwa lengo la kupakua au kupakia bidhaa kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

Usafi wa Soko

20 (1) Kila mfanyabiashara anayefanya shughuli za biashara katika soko atawajibika kuweka eneo lake katika hali ya usafi wakati wote.

(2) Kamati kwa kushirikiana na Mkuu wa Soko itateua siku moja na muda maalum katika juma ambapo soko litafungwa kwa ajili ya kufanya usafi wa jumla.

(3) Kila mfanyabiashara katika soko atatakiwa kushiriki katika usafi wa jumla wa soko bila kukosa.

(4) Kila mfanyabiashara sokoni atatakiwa kufuata Kanuni za Afya.

Huduma ndani ya soko

21 Ni wajibu wa kila mfanyabiashara katika soko kugharamia huduma ya ulinzi, usafi,maji na umeme kulingana na mahitaji yake kila mwezi.

Udhibiti wa

22 Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote:-

nidhamu katika soko

(a) kubandika tangazo au kubandua tangazo lolote bila idhini ya Mkuu wa Soko.
(b) kuweka bendera ya chama chochote cha siasa ndani ya eneo la soko.
(c) kufanya shughuli za kisiasa ndani ya soko.
(d) kuharibu miundombinu ya soko.
(e) kutumia lugha ya matusi ndani ya soko
(f) kufanya shughuli yoyote kwenye eneo ambalo hairuhusiwi au halijajengwa kwa shughuli hiyo.
(g) kupangisha kizimba au eneo la biashara kwa mfanyabiashara mwingine.
(h) kufanya biashara nje ya eneo la soko;au
(i) kutupataka hovyo na kutiririsha maji machafu.

Makosa

23 Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo mtu yeyote:-
(a) hatajisajili kwa Mkuu wa Soko
(b) ataharibu miundombinu ya soko
(c) kufanya biashara kwenye eneo lisilo ruhusiwa
(d) kutupa taka hovyo na kutiririsha maji machafu
(e) kuweka bendera ya chama chochote cha siasa ndani ya soko
(f) kufanya shughuli za kisiasa ndani ya soko
(g) kutolipa ushuru au kodi kwa wakati
(h) kubandika au kubandua tangazo bila idhini ya Mkuu wa Soko
(i) kutumia lugha ya matusi ndani ya soko
(j) kupangisha kizimba au eneo la biashara kwa mtu mwingine
(k) hatashiriki usafi wa soko.
(l) atashusha au kupandisha bidhaa kwenye gari katika muda usioruhusiwa.

Kufifilisha kosa

24 Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi kisichopungua shilingi laki (Tsh.200,000/)na kisichozidi laki tano ( Tsh.500,000) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari

yake mwenyewe na kuwa tayari kujazafomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi na atatakiwa kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Adhabu 25 Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na masharti ya sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili ( Tsh.200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (Tsh.1000,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au vyote kwa pamoja.

## JEDWALI LA KWANZA

## KIBALI CHA KUTUMIA SOKO

Limetungwa chini ya kifungu cha 12

1. Jina la mwombaji…………………………………………………………
2. Anuani ya mwombaji…………………………………………………………
3. Kibali cha…………………………………………………………………
4. Eneo ambalo kibali kitatumika……………………………………………
5. Muda wa kibali ni kuanzia tarehe……………….hadi tarehe…………
6. Masharti ya kutumia kibali;-
   (a) ……………………………………………………………………
   (b) ……………………………………………………………………
   (c) ……………………………………………………………………
   (d) ……………………………………………………………………
   (e) ……………………………………………………………………
7. Tarehe ya kikao kilicho idhinisha kibali……………………………………………
   Muhtasari Na…………………………………………
8. Imesainiwa na:
9. Jina…………………………………………………………………
   Saini…………………………………… …………………
   *Mkuu wa Soko* *Saini ya mwombaji*

Tarehe……………………..…  Tarehe…….……….…….……….…

Mhuri……………………………………………….……….………….………

JEDWALI LA PILI
Limetungwa chini ya vifungu vya 17 na 19

ADA YA KUPANGISHA ENEO

| Na. | Aina ya Chanzo cha Mapato | Kiwango cha Ushuru kwa siku | Kiwango cha Ushuru kwa Mwezi |
|---|---|---|---|
| 1. | Mkungu wa ndizi | 200.00 | |
| 2. | Vibanda | 500.00 | |
| 3. | Bucha | 1000.00 | 30,000.00 |
| 4. | Vizimba | 400.00 | |
| 5. | Wapanga chini | 200.00 | |
| 6. | Vizimba vya kuku | 1000.00 | |
| 8. | Gunia, tenga au kiroba | 300.00 | |
| 9. | Maduka | 500.00 | |
| 10. | Nafaka | 500.00 | |
| 11. | Vibanda vya Simu | 500.00 | |
| 12. | Lishe | 500.00 | 5 |
| 13. | Eneo la matenga | | 50,000.00 |
| 14. | Machinjio ya kuku | | 150,000.00 |
| 15. | Hifadhi ya mizigo | | 100,000.00 |
| 16. | Ofisi ndani ya soko | | 50,000.00 |
| 17. | Kupakia na kupakua mizigo<br>1. Tani 0 hadi 2.9<br>2. Tani 3 hadi 3.9<br>3. Tani 4 hadi 6.9<br>4. Tani 7 na kuendelea | <br>1,000.00<br>2,000.00<br>3,000.00<br>5,000.00 | |

JEDWALI LA TATU

KUFIFILISHA KOSA

(Limetungwa chini ya kifungu cha 24)cha Sheria Ndogo hizi

Mimi…………………………………………wa S.L.P…………………..nakiri Kwa hiari yangu mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala, kwamba mnamo tarehe ………mwezi………..Mwaka……….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha 24 cha sheria Ndogo za (Ushuru wa Masoko na Magulio)za Halmashauri ya Newala 2018

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha ushuru ninao daiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……………………. Mwezi……….Mwaka……………………

Jina……………………………………………Saini………………………………….

Mbele ya:

Jina…………………………………………...Cheo………………………………….

Saini………………………………………Tarehe……………………

Nembo ya Halmashauri imegongwa katika Sheria Ndogo hizo kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Newala uliofanyika mnamo Tarehe 24 Mwezi wa 04 Mwaka 2018 na Nembo iliyogongwa mbele ya:-

MUSSA M. CHIMAE
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya yaNewala*

L.S

RASHID CHITWANGA. NDEMBO,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Newala*

NAKUBALI,

Dodoma,
27 Agosti 2018

SELEMANI S.JAFO (MB)
*Waziri wa Nchi-OR Tamisemi*